**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**TUME HURU YA TAIFA YA UCHAGUZI**

**MSIMAMIZI WA UCHAGUZI**

**JIMBO LA LINDI MJINI NA MCHINGA**

# TANGAZO LA UCHAGUZI

KWA MUJIBU WA KIFUNGU CHA 69 (1) CHA SHERIA YA UCHAGUZI WA RAIS, WABUNGE NA MADIWANI NA. 1 YA MWAKA 2024, MSIMAMIZI WA UCHAGUZI WA JIMBO LA LINDI MJINI NA MCHINGA ANAWATANGAZIA WANANCHI WOTE WALIOJIANDIKISHA KATIKA DAFTARI LA KUDUMU LA WAPIGA KURA LA TUME HURU YA TAIFA YA UCHAGUZI KUWA: -

1. UCHAGUZI WA RAIS, WABUNGE NA MADIWANI UTAFANYIKA SIKU YA **JUMATANO** TAREHE **29 OKTOBA, 2025**.
2. VITUO VILIVYOTUMIKA KUANDIKISHIA WAPIGA KURA NDIVYO VITAKAVYOTUMIKA KUPIGIA KURA.
3. VITUO VYA KUPIGIA KURA VITAFUNGULIWA **SAA MOJA KAMILI (1:00) ASUBUHI** NA KUFUNGWA **SAA KUMI KAMILI (10:00) JIONI.**
4. VITUO VYA KUPIGIA KURA VYA MAGEREZA VITAFUNGULIWA **SAA MBILI KAMILI (2:00) ASUBUHI** NA KUFUNGWA **SAA TISA KAMILI (9:00) ALASIRI.**
5. PAMOJA NA TANGAZO HILI, KWA KILA KITUO CHA KUPIGIA KURA ZIMEBANDIKWA TAARIFA ZIFUATAZO: -

   i. MFANO WA KARATASI YA KURA YENYE MAJINA NA PICHA ZA KILA MGOMBEA PAMOJA NA NEMBO ZA VYAMA VYAO VYA SIASA KWA UCHAGUZI WA RAIS, WABUNGE NA MADIWANI;

   ii. ORODHA YA MAJINA YA WAPIGA KURA WALIOANDIKISHWA NA TUME HURU YA TAIFA YA UCHAGUZI; NA

   iii. ORODHA YA WAPIGA KURA WALIORUHUSIWA KUPIGA KURA MOJA TU YA RAIS.

WANANCHI WOTE MNAOMBWA KUPITIA TAARIFA HIZO ILI KUTAMBUA MAPEMA VITUO MTAKAVYOPIGIA KURA NA KUONA MFANO WA KARATASI YA KURA.

**MUHIMU:** SIKU YA UCHAGUZI NI LAZIMA MPIGA KURA AFIKE KITUONI NA **KADI YAKE YA MPIGA KURA**.

**KWA MPIGA KURA ALIYEPOTEZA KADI YAKE NA AMBAYE ALIANDIKISHWA KWENYE DAFTARI LA KUDUMU LA WAPIGA KURA**, ATARUHUSIWA KUPIGA KURA ENDAPO ATAFIKA KATIKA KITUO ALICHOPANGIWA AKIWA NA LESENI YA UDEREVA AU PASI YA KUSAFIRIA AU KITAMBULISHO CHA TAIFA (NIDA). MAJINA YA KITAMBULISHO MBADALA ATAKACHOWASILISHA, YAWE YANAFANANA NA YALIYOMO KWENYE DAFTARI LA KUDUMU LA WAPIGA KURA.

IMETOLEWA NA: -

MSIMAMIZI WA UCHAGUZI
**JIMBO LA LINDI MJINI NA MCHINGA**
**TAREHE 19 OKTOBA, 2025**